TANGAZO LA SERIKALI Na .706 la tarehe 02 /12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA PANGALE YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Pangale ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia katika alama ya mpaka ya upimaji P1 iliyopo katika makutano ya barabara ya Nshepa na Sikonge yenye majira-nukta 467741E, 9414925N; baada ya hapo mpaka utafuata barabara ya Nshepa hadi katika alama ya mpaka ya upimaji P2 yenye majira-nukta 467283E, 9415014N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa N92$^{0}$6'8"E kwa umbali wa kilomita 2.3 hadi alama ya mpaka ya upimaji P3 iliyopo barabara ya Nselula yenye majira-nukta 468000E, 9417317N; baada ya hapo

*Tangazo la Serikali na. 706 (linaendelea)*

mpaka utaelekea Mashariki - Kaskazini katika uelekeo wa E90$^{0}$6’0”N kwa umbali wa kilomita 0.8 hadi alama ya mpaka ya upimaji P4 iliyopo barabara ya Sikonge katika majira - nukta 468793E, 9417600N karibu na daraja la mto Kasisi; baada ya hapo mpaka utaelekea Mashariki - Kusini katika uelekeo wa E150$^{0}$10’0”S kwa umbali wa kilomita 1.7 hadi alama ya mpaka ya upimaji P5 iliyopo Shule ya Msingi Kasisi A yenye majira - nukta 470475E, 9417148N; baada ya hapo mpaka utapita pembezoni mwa mpaka wa Shule kuelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa S85$^{0}$5’40”W kwa umbali wa kilomita 2.5 hadi alama ya mpaka ya upimaji P6 iliyopo chini ya mlima Pangale yenye majira – nukta 469156E, 9414617N; baada ya hapo mpaka utaelekea Magharibi - Kaskazini katika uelekeo wa W95$^{0}$6’20”N kwa umbali wa kilomita 1.4 hadi ulipoanzia”.

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*